



Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. MDC/E.70/5/18

Tarehe: 17 Machi, 2021.

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI - AJIRA YA MKATABA WA MUDA MAALUM

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya Morogoro anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi saba (07) za kazi ya ajira ya udereva kwa masharti ya mkataba wa muda maalum.

#### 1.0 NAFASI: DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 07)

##### 1.0.1 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii. Kuwapeleka watumishi kwenye maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari za zote katika daftari la safari "Log –book",
- vi. Kufanya usafi wa gari,
- vii. Kufanya kazi nyingine kama atakavyopangiwa na kiongozi wake zinazohusiana na elimu na ujuzi wake wa kazi.

##### 1.0.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na kuendelea
- ii. Awe na Leseni ya Daraja E au C 1 ya Uendeshaji wa Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- iii. Awe amehudhuria Mafunzo ya Msingi ya Uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na serikali
- iv. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

##### 1.0.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia muundo na ngazi za mishahara ya Watumishi wa Serikali yaani TGS B 1 kwa mwezi.

#### 1.0.4 MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA


- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- iii. Nafasi hizi zitajazwa kwa masharti ya mkataba kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hivyo mwombaji awe tayari kupangiwa na kufanya kazi katika Kituo cha kazi chochote ndani ya Halmashauri kulingana na mahitaji ya kazi.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma walioajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni hawatakiwi kuomba nafasi hizi.
- v. Waombaji waambatishe Maelezo Binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- vii. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and Form VI Results Slips) HAVITAKUBALIWA.
- viii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- x. Waombaji kazi ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi, Wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 31 Machi, 2021.**

Maombi yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya Morogoro,  
S.L.P. 1880,  
**MOROGORO.**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ambayo ni [www.morogorodc.go.tz](http://www.morogorodc.go.tz) pamoja na mbaao za matangazo za Halmashauri zilipo Makao Makuu ya Halmashauri.

Limetolewa na:-



Rehema S. Bwasi

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR  
MOROGORO DISTRICT COUNCIL

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO**